**HOTUBA YA MHE. PROF. IBRAHIM HAMIS JUMA, JAJI MKUU WA TANZANIA SIKU YA UZINDUZI WA WIKI YA SHERIA NCHINI 25 JANUARI, 2025**

**Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne,**

**Wahe. Majaji wa Mahakama ya Rufani,**

**Mhe.Khamis Ramadhan Abdalla, Jaji Mkuu wa Zanzibar,**

**Mhe. Jaji Nestor Kayobera, Rais wa Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki,**

**Mhe. Dkt. Mustapher Mohamed Siyani, Jaji Kiongozi,**

**Wahe. Majaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania na Mahkama Kuu Zanzibar,**

**Wahe. Majaji Wakuu wastaafu na Majaji Wastaafu,**

**Mhe. Jaji Mstaafu Mathew Maimu, Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora,**

**Mhe. Prof. Elisante Ole Gabiriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama,**

**Mhe. Eva Nkya, Msajili Mkuu wa Mahakama,**

**Mhe. Janeth Mayanja,Mkuu Wilaya ya Chamwino,**

**Wasajili, Naibu Wasajili Wakurugenzi na Watendaji wa Mahakama, Mahakimu, Mawakili, na watumishi wa kada mbalimbali mliopo,**

**Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana**

***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!***

## Utangulizi

**Mhe Mgeni Rasmi,** awali ya yote napenda nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukamilisha matembezi ya kilomita 5 na mbio za kujifurahisha za kilomita 10 na hatimaye kukutana hapa kwenye viwanja vya vya Mwalimu Julius Nyerere Dodoma kwa lengo la kuzindua wiki ya sheria itakayohusisha utoaji wa elimu ya sheria kwa wananchi.

Aidha, kwa namna ya kipekee, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa kukubali mwaliko wangu wa kuwa mgeni rasmi katika uzinduzi wa wiki ya utoaji wa elimu ya sheria kwa mwaka 2025 na kushiriki nasi kwenye matembezi haya.

Tunatambua kuwa unazifahamu sana hizi hafla za kila mwaka za kusherehekea WIKI ya SHERIA ikifuatiwa na SIKU YA SHERIA (LAW DAY). Tarehe 3/2/2014 ulikuwa mgeni Rasmi SIKU YA SHERIA, katika hotuba yake ya kukukaribisha, Jaji Mkuu Mohamed Chande Othman, alisema hiyo ilikuwa mara yako ya SABA (7) kuwa mgeni Rasmi SIKU YA SHERI. Tarehe 4/2/2015, ulikuwa mgeni Rasmi SIKU YA SHERIA kwa mara ya nane mfululizo, na ilikuwa mara yako ya mwisho maana kipindi cha Awamu ya Nne kilikamilika mwishoni mwa mwaka huo 2015.

Yapo maeneo mengine MAWILI ambayo unayafahamu sana, ambayo yana uhusiano mkubwa na Kauli Mbiu ya Wiki ya Sheria Mwaka huu 2025. Eneo la **kwanza** ni uzoefu wako wa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

Eneo la **pili** ambalo una historia ndefu ya chimbuko lake, ni PROGRAMU YA MABORESHO YA MAHAKAMA na ushawishi wako kwa Benki ya Dunia. Maboresho ya Mahakama yanayoendelea unafahamu chimbuko lake. Jaji Mkuu Mstaafu Mohamed Chande Othman, katika hotuba yake ya kukukaribisha kama mgeni Rasmi Siku ya Sheria ya tarehe 4/2/2015 anatukumbusha hiyo historia, ninamnukuu:

***"Tunakushuru sana pamoja na kuwa ulikuwa kwenye matibabu kwa kututambulisha kwa Viongozi wa Juu wa Benki ya Dunia, Nov. 2014. Tumeanza mazungumzo nao kwa kushirikiana na HAZINA. Kwa upande wetu napenda kukuhakikishia kuwa viwanja, michoro, mifano (models) na maandalizi mengine yako tayari. Tegemeo letu liliobaki kwenye miradi ya maendeleo ya Mahakama ni wewe, Mh. Rais. Tuwiye radhi kwa kukusumbua tena."***

**Mhe Mgeni Rasmi,**

Kila mwaka Mahakama huadhimisha Siku ya Sheria ikiwa ni kuashiria mwanzo wa shughuli za Mahakama kwa mwaka husika baada ya kumalizika kwa likizo ya Mahakama inayoanza tarehe 15 Desemba na kumalizika tarehe 31 Januari.

Siku ya sheria nchini hutanguliwa na wiki ya sheria ambayo hutumika kutoa elimu ya sheria kwa wananchi kwa lengo la kuwawezesha wananchi kuelewa masuala mbalimbali ya kisheria na hivyo kupambanua stahiki zilizo ndani ya sheria na kutafuta njia za kuzipata.

Kupitia utoaji wa elimu katika ya Wiki ya Sheria, wananchi watapata fursa ya kufahamu Katiba, Sheria, Kanuni, na taratibu zinazohusu haki na wajibu wao. Wananchi watapata pia nafasi ya kushuhudia shughuli mbalimbali zinazofanywa na Mahakama na wadau wake ili kuboresha mazingira ya utoaji haki. Na zaidi wananchi watapata fursa ya kutoa mrejesho wa huduma wanazopokea kupitia maoni yao. Maoni yatakayotolewa yatatumika kama mtaji wa kuboresha utoaji haki nchini.

**Mhe Mgeni Rasmi,**

Wiki ya Sheria ya mwaka huu itanaanza leo, tarehe 25 Januari 2025, na kuendelea hadi tarehe 1 Februari 2025. Siku ya Sheria na kilele cha wiki ya sheria kitakuwa tarehe 3 Februari 2025, hapa Dodoma, na mgeni rasmi atakuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**KAULI MBIU**

**Mhe Mgeni Rasmi**,

Kama nilivyogusia awali, DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO ambayo Mahakama iliitumia kufanya maboresho, itafikia ukingoni tarehe 31/12/2025, na DIRA 2026 itaanza tarehe 1/1/2026.

Kauli mbiu ya Mwaka Huu:

***"Tanzania 2050: Nafasi ya Taasisi Zinazosimamia Haki Katika Kufikia Malengo Makuu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo."***

Inalenga kuikumbusha Mahakama kujipanga ili itekele DIRA 2050. Aidha, Kauli mbiu inazihamasisha taasisi za Haki Madai na kujiweka katika utayari wa kufanikisha malengo makuu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Tunakumbushana kuwa Mahakama, na pia Taasisi za Haki Madai, zina wajibu wa kuhakikisha kwamba mfumo wa sheria na utawala bora unaohitajika utaakisi Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Mhe. Mgeni Rasmi, kabla ya kukukaribisha, napenda kutoa rai kwa wananchi na wadau wote wa Sheria kutembelea sehemu zote zitakazoandaliwa kwa ajili maadhimisho ya Wiki ya Sheria nchini kote.

**Mhe Mgeni Rasmi**

Kwa mara nyingine nakushuru kwa kukubali kuwa mgeni rasmi katika uzinduzi wa Wiki ya Sheria na kushiriki nasi katika shughuli za leo. Kwa heshima naomba sasa kukukaribisha utupatie nasaha zako na hatimaye uzindue maadhimisho ya Wiki ya Sheria 2025.

**Mheshimiwa Rais Mstaafu Karibu sana.**